

NOTISI YA MKUTANO NA KUTHIBITISHA AJENDA TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TATU

1. Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 3 wa Mwalimu Commercial Bank Plc utafanyika katika Ukumbi wa Benk Kuu - Mtwara siku ya Alhamisi, Agosti 22, 2019 saa 5:00 asubuhi
2. Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:
 - 2.1 Kufungua Mkutano
 - 2.2 Kupitishwa kwa Ajenda.
 - 2.3 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Pili wa Mwaka 2018
 - 2.4 Kujadili Yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka 2018.
 - 2.5 Taarifa ya Mwenyekiti
 - 2.6 Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi na kupitishwa kwa taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka 2018.
 - 2.7 Uteuzi wa Wakurugenzi na ada za Wakurugenzi.
 - 2.8 Uteuzi wa Wakaguzi wa nje.
 - 2.9 Mapendekezo ya Marekebisho ya MEMARTS.
 - 2.10 Mengineyo yatokanayo na Mkutano
 - 2.11 Tarehe ya Mkutano ujao.
 - 2.12 Kufungwa kwa Mkutano.
3. Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengee cha 2.10 hapo juu lazima atoe taarifa kwa maandishi siku tatu (3) kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.
4. Mwanahisa atakaeshindwa kuhudhuria ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa niaba yake. Taarifa hizi zitufikie angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano.
5. Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.
6. Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora na Mlimani City Dar es Salaam, na katika ofisi zetu za Mwanza, Morogoro na Mbeya. Pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano.
7. Gharama za usafiri na malazi zitagharamiwa na mwanahisa mwenyewe.